# KILIMANJARO INTERNATIONAL LEATHER INDUSTRIES COMPANY LIMITED

**TAARIFA YA KIKAO CHA WADAU WA SEKTA YA NGOZI**

**TAREHE: 29/09/2020**

**UKUMBI: BOT - MWANZA**

## YALIYOMO

1.0. UTANGULIZI ........ 3
1.1. UFUNGUZI ........ 3
1.2. MALENGO YA KIKAO ........ 4
2.0. UWASILISHWAJI WA MADA NA MAJADILIANO KUTOKA KWA WADAU WA SEKTA YA NGOZI ........ 5
3.0. MAAZIMIO YA KIKAO CHA WADAU WA SEKTA YA NGOZI ........ 6
4.0. HITIMISHO ........ 8

## 1.0. UTANGULIZI

Kampuni ya a Kilimanjaro International Leather Industries Company Ltd (KICL) ilifanya kikao cha wadau wa sekta ya ngozi kwa ajili ya kujadili na kuazimia uzalishaji na upatikanaji wa malighafi bora ya ngozi. Kikao hicho kilifanyika mnamo tarehe 29/09/2020katika Ukumbi wa Benku Kuu Tanzania, Mkoa wa Mwanza, kilichohudhuriwa na wadau mbalimbali akiwemo mgeni rasmi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Bi. Jenister Muhagama, , Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi Prof. Elisante Ole Gabriel, Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda, Biasahra na Uwekezaji, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Naibu katibu Mkuu wizara ya Viwanda Bw. Ludovick J. Nduhiye, Mwakilishi wa Katibu TAMISEMI, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mheshimiwa John Mongela, Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Kilimanjaro International Leather Industries Company Ltd ambaye pia ni Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa PSSSF **CPAT** Bw. Hosea Kashimba, Kamishna Jenerali wa Magereza, Meja Jenerali Suleiman Mzee Wakuu wa Wilaya ya Chato,Moshi Mjini na Geita, Mkemia Mkuu wa Serekali, Taasisi za Serikali DIT, TBS, SIDO, TCCIA na TIRDO, FCC

## 1.1. UFUNGUZI

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Bw. John Mongela akiwa kama mwenyeji wa Mkoa wa Mwanza aliitumia nafasi hiyo kwa kumkaribisha mgeni rasmi Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Wizara ya Uratibu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Muheshimiwa Jenister Muhagama kwa ajili ya ufunguzi wa kikao ambapo pamoja na mambo mengine mgeni rasmi alitoa shukrani za dhati na pongezi kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na Jeshi la Magereza kwa ushirikiano ulio thabiti na kuwezesha ujenzi na uwekezaji mkubwa wa kiwanda cha Kilimanjaro International Leather Industries Co. Ltd. . alisema “Ni katika msingi huo sisi kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu tulielekeza na kusimamia Mfuko wa PSSSF na kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Magereza waweze kuanzisha kiwanda cha bidhaa za ngozi cha Kilimanjaro.”

Pia mgeni rasmi aliwashukuru wadau wote kwa kushiriki katika kikao na kuwaasa namna bora ya kuwasilisha, kujadili na kuazimia kwa pamoja maazimio yanayolenga kujenga, kukuza, kuboresha uzalishaji na upatikanaji wa mali ghafi ya ngozi yenye ubora. Mgeni rasmi aliwataka wadau kwa kupitia kikao hiki kilichowakutanisha Wataalamu wabobezi wa Tafiti na Wataalamu wabobezi watendaji kushirikiana kwa uzoefu wao kwa kusikilizana na kutoa maoni na mpango endelevu ili kuboresha njia bora ya upatikanaji wa ngozi bora na yenye viwango vinavyohitajika.

## 1.2. MALENGO YA KIKAO

Agenda za kikao ziliwasilishwa na Mwenyekiti wa Bodi ya kiwanda cha Kilimanjaro International Leather Industries Company Ltd na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa PSSSF CPAT Bw. Hosea Kashimba, katika hotuba yake fupi ambapo aliwaomba wadau kujikita na kujadili kwa kina mambo yafuatayo;-

- Upatikanaji na uboreshaji wa mali ghafi ya ngozi
- Upatikanaji na ukuzaji wa soko la bidhaa za ngozi
- Kuongeza ufanisi wa utengenezaji wa bidhaa za ngozi

## 2.0. UWASILISHWAJI WA MADA NA MAJADILIANO KUTOKA KWA WADAU WA SEKTA YA NGOZI

Mada na majadiliano kuhusiana na changamoto, majadiliano na uboreshaji wa uvunaji wa mali ghafi ya ngozi ziliwasilishwa na Taasisi mbalimbali za Umma, akiwemo Mkurugenzi Mtendaji wa Kilimanjaro International Leather Industries Co. Ltd, Watendaji wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, NMB, DIT, Mkemia Mkuu wa Serekali, Vikundi na Vyama vya Wafugaji na Wakusanyaji ngozi, na Wataalamu wenye uzoefu na muda mrefu ambapo walijikita zaidi katika kuainisha changamoto zinazokabili uvunaji bora wa malighafi za ngozi, na njia bora za kusaidia kutatua changamoto hizo ili kuwezesha uvunaji we viwango na kuzalisha ngozi bora. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo;-

- Hali ya hewa na mazingira inachangia kwa kiasi kikubwa kushusha thamani na ubora wa mali ghafi ya ngozi
- Upigaji holela wa chapa ya ngombe kwa kutumia vifaa vyenye ncha kali, visu, mihuri ya moto na kadhalika
- Upatikanikaji hafifu wa madawa ya mifugo, na ngozi inachangia kwa kiasi kikubwa kushusha thamani na ubora wa ngozi
- Matumizi ya teknolojia duni yanayotumiwa na wavunaji kama machinjio ya kienyeji yenye sakafu ya vumbi, na tekinolojia duni ya upimaji mali ghafi ya ngozi
- Dhana duni ya wafugaji kuthamini sana nyama kuliko malighafi ya ngozi
- Upatikanaji hafifu wa vifaa vya uvunaji kama maji safi ya kutosha, visu vyenye viwango, machinjio ya kisasa, maghala yenye viwango na ubora, majosho ya kuogeshea ngombe, madawa ya kutibia mifugo na ngozi, na kuongezwa ranchi za taifa ili kuongeza thamani na upatikanaji wa mali ghafi ya ngozi
- Kukosekana kwa viwango na madaraja thabiti vinavyohitakijika katika soko la dunia
- Ukosekanaji wa sera madhubuti itakayosimamia uzalishaji bora na viwango vya mali ghafi ya ngozi inayohitajika kwa kuzingatia ubora na viwango vya kitaifa na kimataifa

- Jamii kuthamini zaidi bidhaa mbadala wa ngozi na zinazotoka nje ya nchi na pia kuwa na dhana potofu kuwa bidhaa kutoka nje ni bora kuliko bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi.
- Kutokuwepo kwa elimu madhubuti na hamasa kwa wazalishaji wa mali ghafi ya ngozi na kuepuka fikra potofu zinazosababisha kushuka kwa thamani na ubora wa ngozi
- Kutokua na Mitaji ya kifedha inayowawezesha wafugaji na wavunaji
- Kutokua na wataalamu (Madaktari) wenye ujuzi wa kutosha katika machinjio ili kusimamia uvunaji bora wa ngozi
- Kutokuwepo kwa ushirikiano wa pamoja kwa mamlaka za serikali na hivyo kusababisha migongano na migogoro katika kusimamia taratibu na sheria.
- Wadau kutokupewa elimu ya kutosha katika maeneo yao ya kazi, semina na mafunzo mbalimbali za uboreshaji, uendelezaji na uvunaji wa ngozi. Pia kutokupewa elimu ya kutosha juu ya sheria na kanuni zinazosimamia uvunaji wa ngozi.

## 3.0. MAAZIMIO YA KIKAO CHA WADAU WA SEKTA YA NGOZI

Baada ya uwasilishwaji wa mada mbalimbali na kuainisha changamoto zinazoikabili sekta ya ngozi, wadau waliaazimia kwa pamoja njia ya kutatua changamoto hizo kama ifuatavyo;-

i. Kuwepo kwa madaraja katika ngozi kuanzia Grade I hadi 4

ii. Upatikanaji wa madawa na Vifaa
    - Wizara ya Mifugo itahakikisha utoaji wa ruzuku za dawa kwa ajili ya majosho pamoja na utoaji wa visu maalum
    - Chanjo na tiba kusaidia katika magonjwa ya ngozi

iii. Kutoa elimu juu ya ubora wa ngozi na bidhaa za ngozi kwa wadau ili waweze kujua thamani ya zao la ngozi (TAMISEMI, KLICL, Wizara ya Mifugo) kujua thamani ya zao la ngozi kwani ngozi ni bora kuliko nyama.

iv. Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia TANTRADE, kutengeneza masoko kwa ajili ya bidhaa za ngozi kwa masoko ya ndani na Nje

v. TAMISEMI kutoa waraka kwa wakurugenzi wa Halmashauri kuanzisha maghala kwa ajili ya uhifadhi wa ngozi

vi. Kutumia tekinolojia iliyo bora kama machinjio za kisasa, nyenzo sahihi, na usindikaji bora wa ngozi ili kupata malighafi ya ngozi yenye ubora na viwango.

vii. Kuteua na kusajili mawakala wataowasilisha Ngozi bora.

viii. Kuendeleza Sekta ya Ngozi kwa kuzingatia pia utunzaji wa Mazingira

ix. Wizara ya Mifugo kuhakikisha kuwa zinakuwepo ngozi bora za Kutosha

x. OR TAMISEMI ihakikishe kuwa Vijana, Wanawake na Wenye Ulemavu wanapata upendeleo maalum ya kupata mitaji kutoka kwenye fungu la 'Own Source' ili kuhakikisha wanafanya ufugaji wa Kisasa tupate Ngozi bora.

xi. Wadau wote vikiwepo vyama vya wadau ( mfano: UWANGOTA, LART, TALEPPA, n.k) washiriki kikamilifu kwenye mnyorororo wa thamani wa Ngozi ili kudumisha 'thamani' katika ngozi Wateja wananunua thamani)

xii. Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo) iangalie uwezekano wa kuwepo bodi ya Ngozi kama ambavyo kuna Bodi ya Nyama na Bodi ya Maziwa AU kuwepo na Bodi moja ambayo itasimamia mazao yote ya mifugo (Nyama, Maziwa na Ngozi).

xiii. Wizara ya Fedha kupitia-TRA ione namna bora ya kuwapatia wawekezaji wa ndani nafuu ya uwekezaji (Investment Incentives)

xiv. Kwenye mazao ya ngozi kuwepo na mkakati maalum kuhakikisha kuwa hakuna kitu kinachotupwa, hata mabaki ya ngozi yatumike.

xv. Watanzania waendelee kuhimizwa kutumia bidhaa za Tanzania, na

xvi. Kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, viwango vilivyoandaliwa na TBS vitumike ipasavyo ili kufikia ubora wa kitaifa na kimataifa.

## 4.0. HITIMISHO

Mwenyekiti wa kikao alifanya majumuisho kwa kuwaahidi wadau kuwa changamoto na maoni yote yaliyowasilishwa na wadau yamechukuliwa kwa ajili ya utatuzi na uboreshaji zaidi. Pia aliwaasa Uongozi wa Kampuni kufanyia kazi maoni yote ya wadau na kujikita zaidi katika misingi ya nguzo kuu za masoko ili kutanua wigo zaidi wa masoko na kupata faida. Kwani kuwekeza ni jambo moja, kutunza uwekezaji na kubaki kwenye soko ni jambo jingine na ndio muhimu zaidi. Mwisho, Mwenyekiti alifunga kikao kwa kuwashukuru wadau wote walioudhuria na kuwaambia kiwanda kipo tayari kwa uzalishaji na kuomba wadau wote watoe ushirikiano.